*Jina la mwanafunzi: ...............................................................................* *Shule: ..............................................*
*Mkoa..............................................................................* *Wilaya: ..............................................*

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA

## MTIHANI WA KWANZA WA UPIMAJI DARASA LA NNE FEBRUARI 2025

**Muda: Saa 1:30** **JIOGRAFIA NA MAZINGIRA**

### SEHEMU A: (Alama 30)

**1. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha uiandike katika mabano.**

i. Ipi si aina ya ramani miongoni mwa zifuatazo?
A: Ramani za jumla B: Ramani za topografia
C: Ramani za kisiasa D: Ramani za rangi [ ]

ii. Ni madhara gani ya kimazingira yanaweza kutokea ikiwa watu watachoma misitu?
A: Udongo utabadilika kuwa mweusi B: Majani mapya yataota
C: Moto utawaka kwa muda mrefu D: Ukame na kupotea kwa rutuba [ ]

iii. Milima ya usambara inapatikana katika mkoa upi miongoni mwa ifuatayo?
A: Kilimanjaro B: Tanga C: Mbeya D: Morogoro [ ]

iv. Kipi kati ya vifuatavyo ni chanzo cha uchafuzi wa maji?
A: Kupanda miti karibu na vyanzo vya maji
B: Kuondoa taka karibu na vyanzo vya maji
C: Kuweka chupa za plastiki karibu na vyanzo vya maji
D: Kuondoa taka katika mifereji ya maji [ ]

v. Kipi kati ya vipengele vya ramani vifuatavyo huonesha uhusiano wa umbali uliotumika katika ramani na umbali halisi katika ardhi?
A: Skeli B: Ufunguo C: Kichwa cha ramani D: Fremu [ ]

vi. Ukisafiri kuelekea jua linakozama, unaelekea upande gani wa dunia?
A: Kaskazini B: Kusini C: Mashariki D: Magharibi [ ]

vii. Nini faida ya kuwepo kwa alama za ramani?
A: Husaidia kuelezea vitu halisi kwa urahisi.
B: Husaidia vipofu kuelewa ramani bila shida.
C: Hungárisha ramani na kuipendezesha.
D: Huongeza ukubwa wa ramani. [ ]

viii. Kipi kati ya vitu vifuatavyo si cha asili katika mazingira yetu?
A: Mlima B: Barabara C: Mto D: Bonde [ ]

ix. Bainisha sifa zinazotofautisha mlima na kilima.
A: Miamba na udongo B: Uchache na wingi wa theluji
C: Kimo na mteremko D: Kimo na rutuba ya udongo [ ]

wazaelimu.com

*Jina la mwanafunzi: ……………………………………………………………………* *Shule: …………………………………………….*
*Mkoa……………………………………………………………….* *Wilaya: …………………………………………….*

x. Upi ni umuhimu wa shughuli za kilimo?
A: Hutusaidia kupata maji
B: Hutusaidia kupata chakila na malighafi
C: Husaidia katika upatikakani wa nvua
D: Husaidia kupata sehemu za kustarehe [ ]

2. Oanisha kipengele katiaka **Orodha A** na kipengele sahihi kutoka akatika **Orodha B**

| **Orodha A** | **Majibu** | **Orodha B** |
|---|---|---|
| i. Kagera, Kilimanjaro, Arusha, Mbaya, Ruma na Songwe | [ ] | A: Tumbaku |
| ii. Ruvuma, Tabora, Katavi na Iringa. | [ ] | B: Korosho |
| iii. Tanga and Morogoro | [ ] | C: Chai |
| iv. Mtwara na Pani | [ ] | D: Mkonge |
| v. Njombe, Tanga, Iringa and Mbeya | [ ] | E: Pamba |
| | | F: Kahawa |

**SEHEMU B: (Alama 10)**


**3. Andiaka jibu sahihi katika nafasi ulizopewa katika vipengele (i) – (v)**

i. Nini madhara ya uharibifu wa misitu?
a) ……………………………………………………………………………………………………………
ii. Taja faida moja ya milima na vilima………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
iii. Ni njia zipi zinaweza kutumika kutunza ardhi katika mazingira yetu? Taja njia mbili.
a) ……………………………………………………………………
b) ……………………………………………………………………
iv. Ni aina ipi ya ramani inafaa kwa shughuli za kilimo na biashara?
……………………………………………………………………………………
v. Taja ziwa moja linalopatikana katika bonde la ufa la Afrika Mashariki.
……………………………………………………………………………………………………


wazaelimu.com

**SEHEMU C: (Alama 10)**


**4. Chunguza alama zinazotumika kuwakilisha vitu halisi kisha uandike majina yake.**



i. ………………………………..




ii. ………………………………..



**iii.** ………………………………..



iv. ………………………………..



v. ………………………………..